

Utaratibu wa utoaji vibali vya ujenzi mijini unasimamiwa na sheria ya Mipango Miji (Na. 8 ya 2007) na Kanuni za Ujenzi mijini (Sura 101 ya 1936)

Sheria ya Mipango Miji kifungu 32 (1) kinamtaka mtu kupata kibali cha kuendeleza ardhi kutoka mamlaka ya upangaji, kwa kujaza fomu maalum zilizoainishwa na kanuni za sheria hii. Kifungu 33 (1) kinaweka wazi kuwa iwapo kibali cha kuendeleza ardhi kimetolewa na shughuli za uendelezaji ardhi kutokamilika katika kipindi cha miaka mitatu (3), kibali hicho kitahesabiwa kuwa kimeisha muda wake, na kifungu 33 (2) kinaipa madaraka mamlaka ya upangaji kuongeza muda wa kibali hicho kwa kipindi ambacho inaona kitafaa.. Kifungu 34 (1) kinasema kuwa mtu yoyote Yule atakayekiuka maelezo yaliyopo kwenye vifungu namba 29, 30, 31, 32, 33, na 34 atastahili kupigwa faini kila siku kama itakavyoainishwa

kuwa kibali hicho kimefutwa na itachukuliwa kuwa hakuna kibali chochote cha ujenzi kilichowahi kutolewa kwenye eneo hilo

Wakati wa kuomba kibali cha ujenzi, muombaji anatakiwa awasilishe vitu vifuatavyo:

- i. Nakala ya kibali cha kumruhusu kuendeleza ardhi,
- ii. Uthibitisho wa umiliki wa ardhi anayoombea kibali
- iii. Ramani ya nyumba ikionyesha mpangilio wa matumizi (vyumba) pamoja na vipimo vyake (Ground Floor Plan)
- iv. Ramani ya mkato wa nyumba (Cross – Section)
- v. Ramani za muenekano wa nyumba kwa pande zote nne (Elevations)
- vi. Ramani inayoonyesha mkao wa viwanja kwenye eneo hilo (Block Plan)
- vii. Ramani inayoonyesha mkao wa nyumba kwenye kiwanja (Site Plan)
- viii. Ramani inayoonyesha mifumo ya Miundombinu ya majitaka Septic Tank and Soak away pits)
- ix. Ramani inayoonyesha jinsi Bati litakavyopauliwa (Roof Plan)
- x. Kwa majengo ya ghorofa na majengo yenye upana mkubwa zaidi itatakiwa kuwasilisha na ramani za mfumo wa nguzo na bim (Structural Drawing) pamoja na mahesabu yake.
- xi. Ramani zote ziwe zimegongwa muhuri na Msanifu Majengo aliyesajiliwa na Mhandisi aliyesajiliwa.

na Waziri katika kipindi chote ambacho ukiukaji huo unaendelea.

Kifungu cha 4 kinasema kuwa mtu yoyote Yule hawezi kuanza shughuli ya ujenzi wa jengo lolote lile hadi pale atakapokuwa na :

- a) Aombe kwenye mamlaka ya upangaji kupitia fomu maalumu itakayopatikana kutoka kwenye mamlaka hiyo.
- b) Awasilishe kwenye mamlaka ya upangaji ramani na nyaraka nyingine zote zinazotakiwa kama ilivyoainishwa kwenye kanuni hii, na
- c) Kupata kutoka kwenye mamlaka ya upangaji kibali kilichoandikwa kitakachoitwa "Kibali cha Ujenzi" cha kujenga jengo.

Marekebisho yoyote yanayotarajiwa kufanyika kwenye ramani zilizotolewa kibali lazima yawasilishwe kwenye mamlaka ya upangaji kwa utaratibu ule ule uliotumika kuwasilisha ramani za mwanzo na hakuna mabadiliko yoyote kufanyika hadi pale yatakapoidhinishwa na mamlaka ya upangaji na kuidhinishwa kwenye kibali cha ujenzi cha mwanzo.

Kifungu cha 11 kinamtaka mtu aliyepewa kibali cha ujenzi awe ameanza ujenzi ndani ya miezi sita (6) tangu tarehe ya kutolewa kwa kibali hicho cha ujenzi. Iwapo atashindwa kuanza ujenzi ndani ya muda huo itahesabika